SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR
OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS

# MICHEWENI
# MPANGO WA KUJIANDAA NA KUKABILIANA NA MAAFA

Mei, 2012

## DIBAJI

Wilaya ya Micheweni inakabiliwa na majanga mengi ikiwa ni pamoja na ukame, ajali za barabarani na baharini, mmong'onyoko wa fukwe, na uingiaji wa maji ya bahari katika maeneo ya kuishi na kilimo. Yote haya yanaweza wa kusababisha athari mbaya kwa huduma za kijamii, kiuchumi, kiikolojia, kimazingira na kiafya. Idara ya Kukabiliana na Maafa, katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, ina wajibu wa kutambua majanga hayo na ili iweze kuandaa mipango itakayoweza kukabiliana nayo kwa ufanisi ili kuokoa maisha na mali za watu. Ili kukabiliana na majanga kwa ufanisi Idara ya Kukabiliana na Maafa kwa kushauriana na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Micheweni imeandaa Mpango wa Kujiandaa na Kukabiliana na Maafa wa Wilaya ambao unatoa miongozo ya namna ya kujiandaa na kukabiliana na majanga ya aina zote yanayotokea na yanayotarajiwa kutokea katika wilaya hii pamoja na shehia zake.

Mpango wa Kujiandaa na Kukabiliana na Maafa wa Wilaya ya Micheweni (MKKMM) ni mpango utakaotumika kwa majanga yote ambao umeainisha hatua zinazostahiki kuchukuliwa katika hali ya dharura au maafa makubwa. Mpango huu utawezesha kuwa na uratibu mzuri wa kazi za kujiandaa na kukabiliana na dharura ikiwa ni pamoja na utoaji wa rasilimali na huduma muhimu ili kuweza kukabiliana na matokeo yoyote ya hali ya dharura na/au maafa. MKKMM unaelezea hali halisi ya maafa, mipango ya baadae, namna ya kuyashughulikia maafa, madhara na tathmini ya hatari ya maafa, na kugawa majukumu ya kitaasisi katika wilaya. Mpango huu unaelezea hatua zinazopaswa kuchukuliwa kabla, wakati na baada ya maafa kutokea ikiwa ni kama mkakati mkuu wa kujiandaa, kujikinga na kukabiliana na maafa.

Mpango huu umeandaliwa kwa njia ya kupata maoni ya wadau muhimu kutoka idara mbalimbali za Serikali zilizomo ndani ya wilaya, shehia, mashirika na taasisi zizizo za kiserikali pamoja na mashirika ya kujitolea. Idara ya Kukabiliana na Maafa katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais inathamini sana mashirikiano kutoka kwa wadau hao walioshiriki katika mchakato mzima wa kuandaa Mpango huu. Shukurani za kipekee ziende kwa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Watoto (UNICEF) kupitia Mpango wa UNDAP kwa kutoa msaada wa kifedha na kiufundi katika kutekeleza mradi huu.

**YALIYOMO**


| | | |
|---|---|---|
| DIBAJI | | ii |
| ORODHA YA MAJEDWELI | | v |
| ORODHA YA VIFUPISHO | | vi |
| MAANA YA MANENO | | vii |
| SEHEMU YA KWANZA | | 1 |
| 1. | UTANGULIZI | 1 |
| 1.1. | HISTORIA | 1 |
| 1.2. | LENGO | 2 |
| 1.3. | KUSUDIO | 3 |
| 1.4. | UPEO | 3 |
| 2.0 | HALI HALISI | 4 |
| 2.1 | ENEO NA JIOGRAFIA YA WILAYA | 4 |
| 2.2 | Muhtasari wa hali ya majanga | 5 |
| 3.0 | SABABU ZINAZOCHANGIA MICHEWENI KUWA KATIKA HALI TETE KIMAAFA | 7 |
| 4.0 | MAJANGA MAKUU YALIYOWAHI KUTOKEA KATIKA WILAYA YA MICHEWENI | 9 |
| | Jadweli 1: Majanga makuu yaliyowahi kutokea Wilaya ya Micheweni | 10 |
| 4.1 | Uwezekano wa matukio ya majanga katika wilaya ya Micheweni | 11 |
| 5.0 | VYANZO VYA TAARIFA ZA TAHADHARI YA MAJANGA | 11 |
| 5.1 | Ufahamu na taaluma za asili/jadi | 11 |
| 5.2 | Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) | 12 |
| 6 | ATHARI NA UCHAMBUZI WA HALI TETE | 12 |
| 7 | TARATIBU ZA OPERESHENI | 15 |
| SEHEMU YA PILI | | 17 |
| 8.0 | MGAWANYIKO WA MAJUKUMU | 17 |
| 8.1 | UTANGULIZI | 17 |
| 8.2 | MAJUKUMU | 17 |
| 8.3 | Mgawanyo wa majukumu kwa mujibu wa shughuli za taasisi | 18 |
| 8.4 | MGAWANYO WA MAJUKUMU | 20 |
| 8.5 | Uwezo wa wilaya juu ya Rasilimali za maafa | 25 |
| SEHEMU YA TATU | | 27 |
| 9.0 | MKAKATI WA UTEKELEZAJI WA MPANGO | 27 |
| 9.1 | UTEKELEZAJI | 27 |
| 9.2 | MKAKATI MAALUM | 27 |

Kabla ya maafa (wakati wa kujiandaa – kabla ya maafa) ..................................... 27
Wakati wa Maafa ........................................................................................................ 28
Baada ya Maafa .......................................................................................................... 28
KIAMBATANISHO ..................................................................................................... 30
Kazi na Majukumu ..................................................................................................... 30

## ORODHA YA MAJADWELI


| | | |
|---|---|---|
| Jadweli 1: | Majanga makuu yaliyowahi kutokea Wilaya ya Micheweni ........ | 18 |
| Jadweli Namba 2: | Uwezekano wa wakati wa kutokea majanga........ | 18 |
| Jadweli Namba. 3: | Athari za majanga na hali tete ........ | 21 |
| Jadweli Namba 4: | Shughuli za kujiandaa na kukabiliana na maafa ........ | 28 |
| Jadweli namba 5: | Tathmini ya rasilimali za wilaya ........ | 34 |

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| IKM | Idara ya Kukabiliana na Maafa |
| JP | Jeshi la Polisi |
| JKU | Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar |
| JUMAZA | Jumuiya ya Maimamu Zanzibar |
| JWTZ | Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania |
| JUMIKI | Jumuiya ya Uamsho na Mihadhara ya Kiislamu |
| JUMMUMI | Jumuiya ya Uhifadhi wa Misitu na Maliasili Micheweni |
| JUWAKAP | Jumuiya ya Wanawake Kaskazini Pemba |
| JUWAMWAP | Jumuiya ya Wazalishaji Mwani Pemba |
| KIMADO | Jumuiya ya Maendeleo ya Kiuyu Maziwang'ombe |
| KMW | Kamati ya Maafa ya Wilaya |
| KMKM | Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo Zanzibar |
| KONDEO | Jumuiya ya Maendeleo ya Konde |
| KVZ | Kikosi cha Volantia Zanzibar |
| MKKMWM | Mpango wa Kujiandaa Kukabiliana na Maafa wa Micheweni |
| MKKMMZ | Mpango wa Kujiandaa Kukabiliana na Maafa wa Zanzibar |
| MISCO | Jumuiya ya kutoa huduma za kijamii ya Micheweni |
| MKP | Jumuiya ya Madereva Kaskazini Pemba |
| NGENARECO | Jumuiya ya Uhifadhi wa Rasilimali na Mazingira ya Ngezi |
| TMA | Mamlaka ya Hali ya Hewa |
| UNDAP | |
| UNICEF | |
| ZACPO | Jumuiya ya wakulima wa Karafuu Zanzibar |
| ZAWA | Mamlaka ya Maji ya Zanzibar |
| ZCT | Kamisheni ya Utalii Zanzibar |
| ZDCS | Zanzibar Disaster Communication Strategy |
| ZECO | Shirika la Umeme la Zanzibar |
| ZNCCIA | Jumuiya ya Wafanyabiashara, Wenyeviwanda na Wakulima Zanzibar |
| ZPC | Shirika la Bandari la Zanzibar |

**MAANA YA MANENO**

**MAAFA:** Ni tukio kubwa linalotokea na kuleta madhara kwa jamii, na mazingira yake, tukio ambalo huvuruga utaratibu na mwenendo mzima wa shughuli za kawaida na jamii husika kushindwa kukabiliana na tukio hilo kwa kutumia rasilimali walizonazo (MKKMZ, 2011). Sheria ya Kukabiliana na Maafa Nam. 2 ya mwaka 2003 imeeleza maafa kuwa ni tukio au matukio yanayotokea kimaumbile au yanayosababishwa na binaadamu ambayo husababisha madhara makubwa na kupelekea kuvurugika kwa maisha ya kawaida na kuwafanya watu wahitaji msaada kutoka sehemu nyengine, msaada huo ni pamoja na ulinzi, chakula, nguo, makaazi, huduma za kijamii na afya, na nyenginezo.

**MAAFA YA ASILI:** Ni maafa yanayotokea kutokana na majanga ya kimaumbile kama vile tetemeko la ardhi, vimbunga, mafuriko, ukame, na maradhi ya mripuko (Sheria ya Kukabiliana na Maafa Nam.2 ya mwaka 2003)

**MAAFA YANAYOSABABISHWA NA BINAADAMU:** Ni maafa yanayotokea kutokana na vitendo vya kibinaadamu na kusababisha madhara makubwa kama vile migogogro ya kijamii, vita, kuvuja kwa mafuta, msongamano wa wakimbizi, ajali za viwandani na ajali zinazotokana na vyombo vya usafiri.

**KUJIANDAA NA MAAFA:** Ni shughuli zinazofanywa kwa lengo la kulinda maisha ya watu na mali zao kutokana na hatari zinazotokea au zitakazotokea ambazo haziwezi kudhibitiwa kwa kujikinga. Hivyo, shughuli za kujiandaa zinazingatia kuwa majanga yapo na yanaweza kutokea wakati wowote na hivyo suala la kuweka mipango, nyenzo na taratibu za kukabiliana na majanga hayo kabla ni muhimu. Mipango na taratibu hizi hazikuwekwa tu kwa ajili kuharakisha huduma za kukabiliana na maafa lakini pia husaidia katika kutoa muongozo wakati wa kurudisha hali za jamii baada ya matukio (MKKMZ, 2011).

**KUREJESHA HALI BAADA YA MAAFA:** Ni shughuli zinazoanza mara tu baada ya kukamilika kwa shughuli za kukabiliana na tukio mpaka wakati ambao jamii husika hurudi katika hali zao za kawaida. Wakati mwengine kipindi hiki huwa kinachukua muda mrefu kukamilika kwake. Lengo la shughuli hizi ni kurudisha kwa haraka miundombinu iliyoharibika kama vile maji, mitaro, na huduma za umeme, simu usafirishaji. Madhumuni makubwa ya shughuli hizi ni kuifanya jamii iliyoathiriwa na maafa kurudi katika hali ileile iliyokuwa kabla ya tukio au iliyo bora zaidi. Miongoni

mwa shughuli za kurudisha hali baada ya maafa zinahusisha uondoshaji wa mabaki na kufanya sehemu iliyoathirika iweze kufikika, kurejesha shughuli za kiuchumi, kurejesha huduma za kiserikali na kijamii, kuweka utaratibu wa kuwahudumia waathirika wa janga hasa huduma za makaazi, nguo, na chakula. Pia shughuli za ujenzi hasa wa majengo makubwa, barabara, madaraja, na mabwawa pamoja na kufufua uchumi (MKKMZ, 2011)

**DHARURA:** Ni tukio linalohusisha madhara madogo katika jamii ambapo mara nyingi husababisha vifo au majeruhi kidogo na pia uharibifu kidogo wa mali. Matukio haya ni kama yale ya kugongana kwa magari, kupasuka kwa mabomba ya gesi, na kuungua nyumba moto. Matukio ya dharura ni yale ambayo yanaweza kushughulikiwa kwa kutumia rasilimali za eneo linalihusika (MKKMZ, 2011).

**KITUO CHA OPERESHENI WAKATI WA MAAFA (KOM):** Ni sehemu maalum ambayo imewekwa vifaa muhimu vya mawasiliano ambapo maofisa wa Serikali hutoa na kupokea taarifa, miongozo na kuratibu rasilimali muhimu wakati wa maafa (MKKMZ, 2011).

**KUKABILI MAAFA:** Ni shughuli zote zinazofanyika mara tu baada ya kutokea kwa tukio la maafa hadi hali ya taharuki iliyotokea na tukio hilo itakavyotulia. Lengo kubwa la kukabiliana na maafa ni kuokoa maisha ya watu na mali zao kwa kutoa huduma na bidhaa za muhimu kama vile kuhudumia majeruhi kwa kuwapa huduma za afya, kutoa chakula, maji na makaazi ya dharura. Baadhi ya shughuli zinazofanywa ili kupunguza madhara ya tishio la hali ya maafa ni pamoja na kuliweka eneo la maafa kuwa salama, kuhama maeneo hatarishi, kutafuta na kuokoa majeruhi, kutoa huduma za afya na makaazi watu waliohamishwa katika maeneo mengine na majeruhi. Wakati huu pia hutumika kwa waratibu wa masuala ya maafa kuendelea kufanya tahmini ya awali kwa madhara yaliyotokea pamoja na kuratibu upokeaji wa misaada na vifaa ili kuweza kugawiwa na kutumika kwa haraka katika maeneo yanayohitaji (MKKMZ, 2011).

**KUHAMISHA:** Ni operesheni maalum ambayo ama watu wote au sehemu ya watu waliopata maafa huondoshwa na kuwekwa katika eneo jengine la muda lililo salama.

**JANGA:** Ni tukio linaloweza kuleta athari au madhara na kusababisha kifo au majeraha kwa binaadamu, mali zake, mazingira na jamii kwa jumla.

**HALI HATARISHI:** Ni uwezekano wa kutokezea kwa madhara (vifo, majeraha, kupotea kwa mali, kuporomoka kwa uchumi na mazingira) kutokana na maingiliano baina ya majanga ya asili na yale yanayosababishwa na binaadamu pamoja na hali tete ya eneo au jamii husika.

**HALI TETE:** Ni hali inayotokana na mazingira ya mtu au jamii kuwa katika uwezekano wa kukumbwa na kuathirika na madhara yanayotokana na majanga na huwa na uwezo mdogo wa kugundua na kukabiliana nayo.

**HALI TETE YA KIJAMII:** Ni hali ambayo humpata mtu au kundi la watu ambayo hupelekea kutokuwa na uwezo wa kugundua majanga, kukabiliana na majanga na kurejesha hali baada ya maafa kutokea. Hali hiyo huweza kubadilika kutokana na wakati (MKKMZ, 2011)

**TARATIBU ZA OPERESHENI:** Hii ni miongozo inayoonyesha namna bora ya kutekeleza kazi au majukumu. Miongozo hii huandaliwa katika ngazi ya Idara au Shirika.

## SEHEMU YA KWANZA

## 1. UTANGULIZI

### 1.1. HISTORIA

Mpango wa Kujiandaa na Kukabiliana na Maafa wa Wilaya ya Micheweni (MKKMM) ni mpango ulioanzishwa na Idara ya Kukabiliana na Maafa kutokana na maelekezo ya Sheria ya Maafa Nam.2 ya mwaka 2003, na Sera ya Kukabiliana na Maafa ya mwaka 2011. Katika jitihada za kujiandaa na kukabiliana na maafa pamoja na kupunguza mateso yanayotokana na majanga, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, imeandaa Mpango wa Kujiandaa na Kukabiliana na Maafa Zanzibar. Mpango huo kimsingi unalenga katika kuiwezesha nchi kuweza kujiandaa na kukabiliana na maafa katika ngazi ya taifa. Hata hivyo, kutokana na kuwa asili ya majanga na namna ya kujiandaa na kukabiliana nayo huwa yanatofautiana baina ya sehemu moja na nyengine, mipango kwa ajili ya kujiandaa na kukabiliana na majanga hayo lazima pia kuwa tofauti. Hivyo, Idara ya Kukabiliana na Maafa ilikuja na pendekezo la kuwa na Mipango ya Kujiandaa na Kukabiliana na Maafa ya Wilaya hasa kwa wilaya zile zilizo katika hatari ya kukumbwa na majanga mara kwa mara. Utaratibu huu utafanya kazi katika mfumo wa mipango ya kujiandaa na kukabiliana na maafa wa kila wilaya. Mpango huu utajenga uwezo wa wilaya na jamii kwa jumla katika kukabiliana na maafa ili kupunguza upotevu wa maisha ya watu na mali zao pamoja na mtafaruku wa jamii wakati wa maafa.

Mpango wa Kujiandaa na Kukabiliana na Maafa wa Wilaya ya Micheweni (MKKMM) unaelezea hatua zitakazochukuliwa na maofisa wa Serikali, Taasisi zisizo za Kiserikali ikiwa ni pamoja na sekta binafsi, mashirika ya kiraia, makundi ya kidini, mashirika ya kujitolea katika ngazi ya wilaya.

MKKMM utakuwa unafanya kazi zake katika ngazi ya Wilaya tu kwa masuala ambayo chini ya uwezo wa wilaya kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Maafa Namba 2 ya mwaka 2003, Sera ya Kukabiliana na Maafa, 2011 na pamoja na nyaraka nyengine za Serikali zinazohusiana na masula ya dharura na kukabiliana na maafa. Mpango huu utafanya kazi wakati maafa yaliyotokea yatakuwa ndani ya uwezo wa wilaya, na wakati hali ikiwa ni zaidi ya uwezo wa wilaya wa kukabiliana nayo, itatangawa hali ya maafa kitaifa na hivyo, Mpango Mkuu wa Kujiandaa na Kukabiliana na Maafa utatumika kushughulikia dharura na hali hiyo. Hivyo, operesheni zote zitafanywa kama ilivyoelekezwa katika Mpango Mkuu wa Kujiandaa na Kukabiliana na Maafa.

Mpango huu hautohusika na kushughulikia matukio yanayotokea kila siku, ambayo hayasababishi matatizo makubwa na kikawaida hushughulikiwa na idara mbalimbali na mashirika ya Serikali ndani ya wilaya. Mpango huu unakusudia kukabiliana na dharura na majanga yanayoleta athari na mateso ambayo waathirika wa matukio hayo hawawezi kuyashughulikia bila kupata msaada kutoka sehemu nyengine.

MKKMM ni mpango unaoshirikisha sekta nyingi na umegawanyika katika sehemu kuu tatu:

(i) Sehemu ya Kwanza ni Utangulizi ambayo inatoa maelezo ya wilaya, lengo la kuanzishwa mpango huu na aina za maafa.

(ii) Sehemu ya Pili ni Mgawanyo wa Mjukumu ambayo inaelezea kazi ya kila mdau juu ya shughuli maalum ambayo ni muhimu kwa kujiandaa na kukabiliana na maafa.

(iii) Sehemu ya tatu ni Utekelezaji wa Mkakati ambayo inaelezea hatua na mikakati ya utekelezaji ambayo ni muhimu katika hatua zote za maafa.

Timu ya Uendeshaji ya Wilaya itaendesha mchakato wa mapitio ya Mpango huu na watashirikiana na Kamati ya Kukabiliana na Maafa ya Wilaya pamoja na Idara ya Kukabiliana na Maafa. Kila idara, shirika, mashirika ya kujitolea na taasisi zisizo za kiserikali iliyopewa kazi maalum itahusika na kufanya mapitio ya sehemu zinazowahusu katika mpango huu. Wataalamu hao watapitia vifungu vyote vinavyohusu taasisi na shughuli zao katika mpango kama itakavyohitajika kutokana na uzoefu katika masuala ya dharura, mapungufu yaliyojitokeza katika ufanyajikazi, na mabadiliko ya muundo wa Serikali na taasisi zinazoshughulikia maafa. Idara ya Kukabiliana na Maafa itasaidia katika kupanga, kufanya mapitio, utekelezaji, ufuatiliaji na ufanyaji wa tathmini ya mpango huu. Ikiwa utatumika vizuri na kufanyiwa mapitio mara kwa mara, mpango huu unaweza kusaidia watendaji wa Serikali katika wilaya kujiandaa na kukabiliana na maafa na kulinda raia kutokana na madhara ya majanga ya asili na yale yanayosababishwa na binaadamu.

## 1.2. LENGO

Lengo la mpango huu ni kuanzisha utaratibu utakaowawezesha wadau mbalimbali wa Wilaya ya Micheweni kwa kuwapa muongozo katika:

(i) Kukinga majanga na kupunguza hali ya kukumbwa na maafa kwa wakaazi wa wilaya kwa maafa yoyote yanayoweza kutokea.

(ii) Kuongeza uwezo wa wilaya katika kulinda raia wake kutokana na athari za majanga katika kuokoa maisha na mali, na kuweza kupata mahitaji ya msingi ya binadamu.

(iii) Kukabiliana na maafa kikamilifu wakati tukio la maafa linapotokea halisi ya dharura yoyote yanayohusiana na uharibifu mkubwa ndani ya wilaya.

(iv) Kuanzisha mfumo ambao utaiwezesha wilaya kuwa na uwezo wa

a. Kujiandaa na kukabiliana na maafa kabla, wakati na baada ya maafa kutokea.
b. Kurejesha maeneo yalioathirika na maafa katika hali ya kawaida
c. Kukinga na kupunguza hali ya kukumbwa na maafa kwa baadae.

## 1.3. KUSUDIO

MKKMM inanzisha taratibu za uendeshaji na miongozo ambayo itawezesha wilaya kuokoa maisha, kupunguza majeraha, kulinda mali, na kuendeleza kazi za Serikali wakati wa hali ya dharura. Mpango huu unatoa miongozo itakayopelekea kufanyika kwa operesheni kwa ufanisi na kwa utaratibu utakaotumia rasilimali zinazomilikiwa au zinazopatikana katika Serikali ya wilaya au ya Taifa. Mpango huu unaonyesha taasisi za kukabiliana na maafa na umeainisha na kugawa majukumu ya kazi za dharura kwa taasisi hizo.

Wahusika wakuu katika mpango huu ni Kamati ya Kukabiliana na Maafa ya Wilaya, Kamati za Maafa za Shehia, idara nyengine za Serikali, taasisi za kiraia, mashirika ya kujitolea, taasisi zisizo za kiserikali pamoja na taasisi nyengine zozote ambazo zinasaidia katika kukabiliana na maafa katika wilaya.

## 1.4. UPEO

Mpango huu utafanya kazi ndani ya mipaka ya Wilaya ya Micheweni tu, pamoja na shehia zote ndani ya wilaya. MKKMM inaeleza hatua ambazo zinapaswa kuchukuliwa ikiwa maafa makubwa au dharura itatokea, au hali nyingine yeyote ambayo itahitaji juhudi za wilaya kuweza kukabiliana nayo, na wakati ambapo msaada ya kitaifa utahitajika ili kuongeza nguvu za wilaya kushughulikia suala hilo.

MKKMM utatumika kwa idara zote, taasisi za serikali, na taasisi zisizo za kiserikali, mashirika ya kujitolea ambazo zinaweza kupewa kazi za kusaidia wakati wa majanga au dharura zozote ndani ya wilaya.

## 2.0 HALI HALISI

### 2.1 ENEO NA JIOGRAFIA YA WILAYA

Wilaya ya Micheweni ipo katika Mkoa wa Kaskazini kisiwani Pemba, na inaundwa na Majimbo 4, Wadi 10, Shehia 27 na inajumuisha visiwa vidogo vidogo 4 (haviishi watu, hutumika kwa kilimo tu) visiwa hivyo ni: Kisiwa Ng'ombe, Mbale, Kamate, Kisiwa Khamisi. Wilaya hii ina eneo lenye jumla ya kilomita za mraba 226. Sehemu kubwa ya wilaya iko katika ukanda wa matumbawe ambao unahusisha sehemu ya kaskazini na mashariki ya kisiwa cha Pemba.

Idadi ya watu (kutokana na makisio ya mwaka 2007)

| | |
|---|---|
| Idadi ya watu: | 103,816. |
| Wanaume: | 50,874 |
| Wanawake: | 52,942 |

**Hali ya hewa**

| Vituo vya kurekodi mvua | 2010 | 2011 |
|---|---|---|
| Matangatuani | 31.65 | 27.6 |
| Makangale | 28.12 | 26.13 |

**Miongo**

Masika: Machi – June

Vuli: Agosti – Novemba

**Viwango ya Joto:**

Juu 320C

Chini 260C

**Kilimo**

Eneo la kilimo

| | |
|---|---|
| Maeneo ya kilimo cha mpunga | 4,600 acres |
| Ardhi ya miamba/mawe | 2530 acres |
| Msitu | 10,050 hectors |

**Sekta ya Afya**

Idadi ya Vituo vya Huduma za Afya (PHCU)

| | |
|---|---|
| First Line. Vituo vya kawaida (Vidogo) | 7 |
| Second Line. Vituo vya kati na kati | 4 |
| Idadi ya Hospiali Ndogo | 1 |
| Huduma za Kibinafsi | 2 (Sizini na Konde) |

**Magonjwa ya Miripuko**

| | |
|---|---|
| Kipindupindu | 381 (2009) |
| Kuharisha | 7913 (2009) |
| | 1092 (2010) |
| | 11,667 (2011) |
| Kuhara damu | 329 (2009) |
| | 520 (2010) |
| | 409 (2011) |
| Ganzi | 151 |

**Sekta ya Elimu**

| | |
|---|---|
| Skuli za Msingi | 15 |
| Skuli za Msingi na Kati | 5 |
| Skuli za Sekondari | 8 |
| Vyuo vya Elimu ya Juu | 1 |
| Skuli za Maandalizi | 4 |
| Usalama | |
| Vituo vya Polisi | 2 |
| Polisi jamii | |

## 2.2 Muhtasari wa hali ya majanga

Wilaya ya Micheweni inakabiliwa na idadi kubwa ya matukio ya majanga ambayo mara nyingi kusababisha athari kubwa kwa maisha ya watu na mali zao. Matukio hayo ni pamoja na ukame, ukataji miti, kutopatikana kwa mazao, kuzuka kwa wadudu waharibifu, muda mrefu wa jua, magonjwa yanayosababishwa na maji machafu pamoja na magonjwa ya milipuko (kipindupindu na surua), kuzuka kwa moto, upepo mkali na ajali za baharini na uingiaji wa maji ya bahari katika maeneo ya kilimo, maeneo hayo baadae huwa hayana rutuba kwa kilimo kutokana na chumvi iliyosababishwa na uingiaji huo wa maji ya bahari. Mengi ya matukio haya yanatokana na shughuli za kibinadamu na baadhi yao ni matokeo ya majanga ya asili.

Upande wote wa mashariki ya wilaya ya Micheweni na sehemu ya Makangale ni ukanda wa matumbawe. Maeneo haya ni moja ya maeneo yaliyo katika hatari ya kukabiliwa na majanga ya aina nyingi hapa Zanzibar. Majanga tofauti kama vile ukame, ajali za baharini, magonjwa ya milipuko kama vile kipindupindu na surua na mengine huripotiwa mara kwa mara katika eneo hilo. Ukataji miti na mahitaji ya ardhi ya kilimo pia pia yamepelekea uingiaji wa maji ya bahari katika maeneo ya kilimo kitu ambacho

kimeathiri shughuli za kilimo katika maeneo mbalimbali ya wilaya ya Micheweni. Mmomonyoko wa fukwe na shughuli za kilimo katika maeneo ya pwani ya wilaya umesababisha maji ya bahari kuvamia mashamba ya mpunga. Maeneo yaliyoathirika zaidi ni Ukele, Koowe, Chamawe, Mwanasoza, Vuleni, Wapape, Fumbi Kuu, Sijuu, Kisiwani, Kwagome, Mjananza, na Chwaka amabyo ni maeneo ya kulima mpunga. Maeneo hayo yamekuwa hayana rutuba kwa ajili ya kilimo kutokana na wingi wa chumvi katika ardhi kulikosababishwa na uvamizi wa maji ya bahari. Sababu nyingi zimetolewa juu ya chanzo cha hali hii, sababu ya wazi zaidi ilikuwa ni upanuzi wa ardhi ya kilimo kwenye sehemu ndogo ya ukanda wa pwani. Mikoko ilikatwa katika maeneo mengi ili kuweza kupata maeneo ya kilimo cha mpunga. Utengenezaji wa chumvi, kufanya chokaa na kukata mikoko kwa ajili ya kuni pia kulitambuliwa kuwa ni sababu kuu za kuchangia matukio ya maji ya bahari kuingia katika mashamba.

Mwaka 2008 wilaya ya Micheweni ilipatwa na ukame mkubwa ambao ulisababisha uhaba mkubwa wa chakula. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na mashirika ya Kimataifa kama vile "Save the Children" na UNICEF ilichukua hatua muafaka juu ya hali hiyo ikiwa ni pamoja na kugawa chakula na kuanzishwa kwa mpango maalum wa kuhamisha fedha. Uzoefu wa ukame wa mwaka 2008 katika ukanda wa Mashariki Kaskazini na sehemu nyingine za wilaya unaleta changamoto kubwa na kuonyesha haja kubwa ya kuwa na mpango wa kujiandaa na kukabiliana na maafa.

Mwaka 2007 sehemu ya mashariki ya wilaya hasa Kiuyu Mbuyuni na Maziwang'ombe zimewahi kukumbwa na ugonjwa wa ajabu ambao ulipewa jina la 'ganzi'. Kulikuwa na vipimo mbalimbali vya kidaktari ili kubaini ugonjwa huu ambao ulichukua siku nyingi kuutambua. Sababu kuu ya ugonjwa huu haikujulikana. Moja ya sababu za magonjwa ya milipuko kama vile kipindupindu, kuhara na kuhara damu ni kutokuwa na/au kutokutumia vyoo. Kwa mujibu wa ripoti kutoka Timu ya Afya ya Wilaya ya Micheweni, familia zenye vyoo ni chini ya 69%, wakati idadi inayotakiwa ni zaidi ya 85%.

Hali tete ya wilaya juu ya kukumbwa na majanga ya asili pamoja na hali tete ya kijamii na kiuchumi kwa watu wanaoishi katika wilaya hii ni changamoto kubwa kwa taasisi za Serikali na hivyo inasisitiza haja ya kuwa na mpango madhubuti wa kujiandaa na kukabiliana na maafa.

## 3.0 SABABU ZINAZOCHANGIA MICHEWENI KUWA KATIKA HALI TETE KIMAAFA

Eneo: Kijiografia, eneo la wilaya ya Micheweni limo katika hali tete ya kukumbwa na majanga kama vile ukame, dhoruba, magonjwa ya milipuko na mengine. Kiasi cha hekta 2530 za wilaya ya Micheweni ni ardhi ya miamba ambayo ni rahisi kukabiliwa na ukame. Wilaya hii imezungukwa na visiwa vidogo vidogo vingi ambavyo haviishi watu ukilinganisha na wilaya nyengine za Zanzibar. Visiwa hivi kikawaida hutumika kwa shughuli za uvuvi na kilimo. Wakulima na wavuvi hawa hupiga kambi kwenye visiwa hivi na kusababisha uharibifu wa visiwa hivyo na hupelekea kutokea kwa majanga mbalimbali ikiwemo ajali nyingi za baharini wakati wa kwenda na kurudi unaosababishwa na upepo mkali na dhoruba.

Hali ya kiuchumi: Wilaya ya Micheweni inategemea shughuli chache za kiuchumi kama vile uvuvi, kilimo, mifugo, uchimbaji wa mawe na biashara ndogo ndogo kwa ajili ya maisha ya watu. Kuna baadhi ya vivutio vya utalii kama vile fukwe na maeneo ya kihistoria ambayo huvutia shughuli za utalii katika wilaya hiyo. Uvuvi, kilimo na biashara ndogo ndogo ni shughuli kuu za kiuchumi zinazofanywa na wakaazi wa wilaya ya Micheweni.

Uchimbaji wa mawe ni moja ya shughuli za kiuchumi ambazo hufanywa katika wilaya hii. Utengenezaji wa matofali ya mawe husababisha uharibifu mkubwa wa mazingira kwa kuacha mashimo makubwa baada ya kuchimba mawe na matofali, ajali nyingi hutokea katika maeneo ya machimbo hayo. Mara nyingi waathirika ni watoto kwa vile ajira za watoto ni za kawaida katika maeneo hayo ya uchimbaji wa mawe. Kiuyu Mbuyuni, Maziwa Ng'ombe na Mjini Wingwi ndiyo maeneo yaliyoathirika zaidi katika wilaya hii.

Hali ya kimazingira: Shughuli za kibinadamu katika sekta mbalimbali mara nyingi huchangia uharibifu mkubwa wa mazingira. Uvuvi na kilimo ni miongoni mwa maeneo yaliyoathirika zaidi katika wilaya ya Micheweni kiasi ambacho kama hakutokuwa na udhibiti inaweza kusababisha maafa makubwa. Aina ya uvuvi uliozoeleka wa 'ngwanda' ni chanzo kikuu cha mmongonyoko wa fukwe na miamba kwa vile hutumia kiasi kikubwa cha mchanga kwa ajili ya kuzamisha nyavu zao. Pamoja na juhudi za Idara ya Mazingira katika Wilaya ya Micheweni kuhamasisha utunzaji wa mazingira na Kamati za Maafa za Shehia kushauri juu ya kukomesha utumiaji wa njia za uvuvi zisizorafiki kwa mazingira, bado matumizi hayo yanaendelea. Shughuli za kilimo katika maeneo

ya ukanda wa pwani wa wilaya pia kuchangia kwa kiasi kikubwa uingiaji wa maji ya bahari katika maeneo ya nchi kavu. Kuchimba mchanga karibu na fukwe na maeneo mengine kwa ajili ya shughuli za ujenzi pia huchangia sana uharibifu wa mazingira. Tumbe ni miongoni mwa maeneo yaliyoathirika kutokana na shughuli hizi ambazo zinapaswa kupigwa vita haraka na pande zote zinazohusika ili kupunguza hatari za kimaafa.

Ongezeko la kasi la idadi ya watu katika wilaya ya Micheweni linaongeza shinikizo katika mahitaji ya nishati ambayo hufanya watu kutafuta vyanzo mbadala vya nishati kama vile kuni. Ukataji mkubwa wa miti kutokana na kilimo cha kuhamahama, uchomaji wa mkaa na ukataji kuni kunaongeza matumizi yasiyokuwa endelevu ya rasilimali za msitu kitu ambacho kinapelekea kuongezeka kwa ukame, mafuriko, mmong'onyoko wa ardhi, na magonjwa. Majanga yanayotokea mara kwa mara katika wilaya hii ni pamoja na ajali za barabarani na baharini ambazo husababisha vifo na majeraha kwa watu wengi.

Athari zinazotokana na mabadiliko ya tabia nchi zimekuwa ni tatizo la kimataifa. Kwa mujibu wa taarifa zilizopatikana kutoka Idara ya Mazingira, ongezeko la kina cha maji ya bahari kumesababisha mmong'onyoko wa fukwe. Mabadiliko haya ya ongezeko la maji ya bahari ni athari zinazotokana na mabadiliko ya tabia nchi.

Umaskini: Kulingana na Ripoti ya Maendeleo ya Binadamu ya mwaka 2005, wilaya hii ndiyo wilaya maskini zaidi Zanzibar ikiwa na kiwango cha umaskini cha 0.109935. Inakadiriwa kuwa zaidi ya 50% ya wakaazi wa wilaya ya Micheweni wana kipato ambacho ni chini ya kipato cha kuweza kukidhi mahitaji ya msingi. Kaya maskini huwa zimo katika hatari zaidi ya kukumbwa na majanga kuliko kaya zenye kipato cha kiasi. Hii ni kwa sababu kaya maskini huwa hazina rasilimali za kutosha za kifedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya matumizi kabla, wakati na baada ya matukio ya maafa. Matokeo yake wanakuwa katika hatari zaidi ya kukumbwa na madhara ya maafa, ikiwa ni pamoja na vifo.

Jinsia: Kuna kaya nyingi zinazoongozwa na wanawake katika wilaya hii kutokana na shughuli za kiuchumi zinazofanywa na wanaume ambao wanatumia muda wao mwingi katika kambi za uvuvi (dago), Unguja, Tanzania Bara na Mombasa, hasa katika jamii za wavuvi katika sehemu ya Kaskazini Mashariki ya wilaya hii. Familia hizi mara nyingi huwa katika wakati mgumu wakati wa hali ya dharura kuliko kaya zinazoongozwa na wanaume. Hii ni kutokana na aina za ajira zilizopo, kipato cha chini na majukumu ya ulezi katika familia.

Elimu: Kiwango cha elimu kwa wakaazi wa eneo hili ni cha chini sana, hali ambayo inaleta athari kubwa katika kukabiliana na maafa. Jamii yenye kiwango cha juu cha elimu inakuwa na uwezo mkubwa wa kukabiliana na maafa kwa haraka ikilinganishwa na jamii yenye kiwango cha chini cha elimu. Hali hii pia inaweza ikawa kikwazo cha kupata na kuelewa taarifa za tahadhari na hatua za kuchukua. Kiwango cha kujua kusoma na kuandika kwa wilaya ya Micheweni ni asilimia 46%, ambacho ndicho cha chini kabisa kwa Zanzibar.

Makundi yenye mahitaji maalum: Makundi yaliyo katika hatari zaidi ya kukumbwa na maafa katika wilaya ya hii ni wazee, watoto, watu wenye ulemavu na watalii ambao hawawezi kuelewa taarifa za tahadhari wakati wa hali ya dharura ambazo hutolewa kwa lugha ya asili ya sehemu husika. Watu wenye mahitaji maalum hutakiwa kupewa kipaumbele katika hali ya dharura ili kuokoa maisha na mali zao.

Magonjwa: Magonjwa ya mlipuko hasa kipindupindu na surua katika wilaya ya Micheweni hutokana hasa na hali duni ya maisha na kiasi kidogo cha uelewa kuhusu chanjo. Baadhi ya kaya huishi katika makaazi yasiyo na vyoo wala hakuna mfumo maalum wa maji taka. Makaazi ya aina hii huwa na sifa ya kutokuwa na huduma ya miundombinu ya kijamii kama vile udhibiti na ukusanyaji wa taka ambao husababisha hatari ya kupata magonjwa ya kuambukiza. UKIMWI unabaki kuwa ni moja ya magonjwa makubwa na yenye madhara makubwa kwa watu wa Micheweni.

## 4.0 MAJANGA MAKUU YALIYOWAHI KUTOKEA KATIKA WILAYA YA MICHEWENI

Wilaya ya Micheweni ipo katika hatari ya kukumbwa na majanga mengi ambayo yana uwezo wa kuiathiri jamii, na kusababisha majeruhi, pamoja na kuharibu mali ya umma au binafsi. Muhtasari wa athari hizi ni kama unavyoonekana katika Jedwali namba 1.

Wilaya ya Micheweni imeshawahi kukumbwa na aina mabalimbali za majanga ya asili na yale yanayosababishwa na binaadamu. Uzoefu unaonyesha kuwa majanga kama vile ukame, magonjwa ya milipuko, moto, upepo mkali, ajali (barabara na baharini), mvua kubwa na mafuriko, na wadudu waharibifu, uharibifu wa mazingira, mmong'onyoko wa fukwe, uingiaji wa maji ya bahari katika maeneo ya nchi kavu ni baadhi ya aina kuu za majanga zilizowahi kutokea katika wilaya hii. Baadhi ya majanga haya yamekuwa yakisababisha upotevu wa maisha ya watu, uharibifu wa mali na

miundombinu, na uharibifu wa mazingira na hivyo kusababisha kurejesha nyuma maendeleo yaliyofikiwa miaka mingi nyuma.

**Jadweli 1: Majanga makuu yaliyowahi kutokea Wilaya ya Micheweni**

| Majanga ya asili | Majanga yanayosababishwa na binaadamu |
|---|---|
| Ukame (Ukanda wa Kaskzini Mashariki) | Magonjwa ya mripuko ( kipindupindu na surua) |
| Ugojwa wa mifugo (new castle) | Ajali za baharini |
| Wadudu waharibifu | Ajali za barabarani |
| Mvua kubwa | Moto |
| Uvamizi wa maji ya bahari | Uharibifu wa mazingira (uchimbaji wa mawe na kukata miti) |
| Mmong'onyoko wa fukwe | |

4.1 Uwezekano wa matukio ya majanga katika wilaya ya Micheweni

Jedwali namba 2 inatoa muhtasari wa uwezekano wa kutokea majanga katika wilaya hii. Mengi ya majanga hayo yanaweza yakatokea na kuweza kusababisha upotevu wa maisha, hasara kubwa ya kiuchumi na kijamii, uharibifu na upotevu wa mali pamoja na matatizo ya kiafya.

Matukio ya majanga haya huwa yanawekewa kumbukumbu kila mwaka ili kuweza kufuatilia na kufikiria athari zinazoweza kujitokeza katika wilaya, na pia kuelewa ni mwezi gani janga fulani linaweza likatokea ili taasisi zinazohusika ziweze kuchukua hatua kama zilivyoelezwa katika mipango yao ya kujiandaa na majanga.

**Jadweli Namba 2: Uwezekano wa wakati wa kutokea majanga**

| AINA YA JANGA | MWEZI WA KUTOKEA JANGA | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | JAN | FEB | MAC | APR | MEI | JUN | JUL | OGA | SEP | OKT | NOV | DIS |
| Ukame | ■ | ■ | ■ | | | | | | | | | ■ |
| Kipindupindu | | | | ■ | ■ | ■ | ■ | | | | | |
| Wadudu waharibifu | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | | | ■ | ■ | ■ | |
| Mvua kubwa na mafuriko | | | ■ | ■ | ■ | | | | | | | |
| Uharibifu wa mazingira | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ |
| Magonjwa ya mifugo | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | | | | | | |
| Ajali za baharini | | | | | ■ | ■ | ■ | | | | | |
| Ajali za barabarani | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ |
| Upepo mkali | | | | | | ■ | ■ | ■ | | | | |
| Mmong'onyoko wa fukwe | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ |
| Uvamizi wa maji ya bahari | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ |
| Moto | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ |
| Chakula chenye sumu | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ |

## 5.0 VYANZO VYA TAARIFA ZA TAHADHARI YA MAJANGA

Kuna vyanzo kadhaa ambavyo taarifa za tahadhari kuhusiana na majanga zinaweza zikapatikana katika wilaya ya Micheweni. Vyanzo vikuu vya taarifa za majanga katika wilaya ya Micheweni ni ufahamu na taaluma za asili/jadi na taarifa za utabiri wa hali ya hewa kutoka Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania ambao hurushwa hewani na vyombo vya habari. Taarifa kutoka mamlaka za Serikali kuu na Serikali za mitaa pia kusambazwa kwa jamii.

### 5.1 Ufahamu na taaluma za asili/jadi

Kuna vyanzo vingi vya upatikanaji wa taarifa ambavyo hutolewa na wazee katika jamii, taarifa ambazo hujulikana kutokana na dalili na ishara zinazohusiana na

viumbe, ndoto, sehemu zilipokaa nyota na mwezi, na mwenendo wa hali ya hewa. Jamii hupata taarifa juu ya hali ya dharura kupitia taaluma za jadi/asili ambazo huashiria aina gani ya habari inatolewa kwa umma kwa kutumia njia za kienyeji kama vile upatu, pembe na nyenginezo. Mfumo wa tahadhari katika wilaya hauko rasmi, ingawa unaweza kusaidia ufanisi wa kujiandaa na kukabiliana na hali kabla na wakati maafa yanapotokea. Taarifa zinazotolewa kwa kutumika ufahamu na taaluma za asili/jadi haujawekwa kwenye kumbukumbu yeyote iliyo rasmi. Hata hivyo, kama ilivyoainishwa na watu wa wilaya ya Micheweni, ikiwa kutawekwa na taarifa hizi na kutumika, itakuwa ni hatua muhimu sana katika jitihada za kujiandaa na kukabiliana na maafa.

### 5.2 Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA)

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania ni chanzo kingine cha taarifa zinazohusiana na utoaji wa tahadhari ya dharura na majanga. Taarifa zinazotoka katika Mamlaka hiyo ni zile zinazohusiana na utabiri wa hali ya hewa ambazo hurushwa hewani kupitia vyombo vya habari vya umma na binafsi kila siku. Hata hivyo hakuna mawasiliano ya moja kwa moja kati ya TMA na vituo vya Redio ya Jamii ya Micheweni na Redio Istiqama ambazo zinasikika sehemu zote za wilaya ya Micheweni na majirani zake. Hivyo, ilipendekezwa kuwa uongozi wa wilaya ufanye mawasiliano na TMA ili kutumia vituo vya redio Jamii vya Micheweni kwa ajili ya taarifa za hali ya hewa na nyengine zote zinazohusiana na maafa.

### Utoaji wa Taarifa za Maafa

Mfumo wa kawaida wa kupeana taarifa ni ule uliozoeleka wa kutoa taarifa kutoka kwa jamii kwenda kwa sheha hadi kwa Mkuu wa Wilaya. Baada ya hapo taarifa hizo husambazwa kwa vyombo vya habari na kwa umma. Hata hivyo, utaratibu huu unategemea kipaumbele na aina ya taarifa. Kwa taarifa za dharura, mfumo huu mara nyingi huvurugika na hivyo kushindwa kufata taratibu hizo na husababisha kuwepo kwa taarifa zisizo sahihi. Wakati wa hali ya dharura mara nyingi husambazwa taarifa za uvumi ambazo huzidisha watu kuingiwa na hofu na kuchanganyikiwa. Ili kuepuka hali hii ni vyema kukawa na utaratibu maalum wa mawasiliano na kufuatwa. Ikiwa janga litatangazwa kuwa ni la kitaifa taratibu zitakazofuatwa ni zile zilizoainishwa Katika Mkakati wa Mawasiliano Wakati wa Maafa.

## 6 ATHARI NA UCHAMBUZI WA HALI TETE

Athari na uchambuzi wa hali tete za maafa utawasaidia maafisa wa mipango wa wilaya kufahamu aina za majanga zilizopo katika wilaya, athari za hali tete na ukubwa wake

kitu ambacho kitawasaidia kupanga namna ya kujiandaa na kukabiliana na maafa. Kila wilaya ina hali yake ambayo hutofautiana na wilaya nyingine, ambayo inahitaji kufanyiwa mapitio mara kwa mara kama itakavyokubaliwa na Idara ya Kukabiliana na Maafa na Kamati ya Kukabiliana na Maafa ya Wilaya. Timu ya mipango ya wilaya itapaswa kupanga mchakato wa kufanya mapitio ili kuweza kubaini matukio yote yatakayojiri ndani ya muda maalum.

**Jadweli Namba. 3: Athari za majanga na hali tete**

| AINA YA JANGA | ATHARI INAYOTARAJIWA KUTOKEA | MAKUNDI YALIYO KATIKA HATARI | SEHEMU ILIYO KATIKA HATARI NDANI YA WILAYA |
|---|---|---|---|
| Ukame | • Ukosefu wa mazao<br>• Unguaji wa msitu na malisho ya wanyama,<br>• Upungufu wa chakula unaosababisha njaa<br>• Kuathirika kwa mfumo wa umwagiliaji maji<br>• Kuathirika kwa vianzio vya maji (visima na chemchem) | • Ng'ombe, punda, mbwa, mbuzi, kondoo, na wanyama wengine, kuku<br>• Binaadamu | Wilaya yote |
| Maradhi ya mripuko | • Kupoteza maisha<br>• kupungua kwa nguvu kazi<br>• Athari za kiuchumi kutokana na kupigwa marufuku kwa usafiri na biashara | Wazee, wanawake na watoto | Wilaya yote ingawa ukanda wa kaskazini Mashariki huathirika zaidi |
| Wadudu waharibifu | • Ukosefu wa mazao<br>• Uhaba wa chakula<br>• Uhaba wa malisho ya wanyama,<br>• Ukosefu wa mbegu kwa msimu inayofuata<br>• Mfumko wa bei za bidhaa<br>• Hali ngumu ya kiuchumi<br>• Utapia mlo | • Jamii<br>• wanyama na mimea | Wilaya yote |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Mvua kubwa na mafuriko | • Ukosefu wa mazao na mifugo<br>• Mmong'onyoko wa ardhi<br>• Upoteaji wa mali (nyumba, mifugo na miti) | • Jamii<br>• wanyama na mimea | Sehemu za chini katika ukanda wa Kusini na Magharibi ya wilaya hiyo |
| Uharibifu wa mazingira | • Ukame na upotevu wa rutuba ya ardhi<br>• Upotevu wa mimea na misitu | • Jamii<br>• wanyama na mimea | Wilaya yote |
| | • Ukosefu wa mvua<br>• Ukosefu wa mazao<br>• Maradhi ya mripuko<br>• Mashimo makubwa yasiyo na matumizi<br>• Kupanda kwa maji ya bahari katika maeneo ya nchi kavu | | |
| Magonjwa ya mifugo | • Vifo vya mifugo<br>• Ukosefu wa protini<br>• Mfumko wa bei<br>• Maradhi ya binaadamu<br>• Athari za kiuchumi kwa wafugaji<br>• Umasikini | • Jamii<br>• Wanyama | Wilaya yote |
| Ajali za baharini | • Kupoteza maisha na mali<br>• Kupoteza nguvu kazi | • Jamii | Wasafiri wanaokwenda na kutoka Pemba kwenda Tanga na Mombasa na visiwa vidogo vidogo ndani ya wilaya |
| Upepo mkali | • Kupoteza maisha na mali<br>• Kuharibika kwa makaazi ya watu<br>• Upotevu wa mazao na miti<br>• Uharibifu wa miundombinu<br>• Kuacha kufanya kazi za kijamii na kiuchumi<br>• Uhaba wa samaki<br>• Kuibuka ugonjwa wa macho<br>• Kushindwa kusafiri. | • Jamii<br>• wanyama na mimea | Wilaya yote |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Mmong'onyoko wa fukwe na kupanda kwa maji ya bahari katika maeneo ya nchi kavu | • Kupoteza vivutio vya utalii<br>• Upotevu wa mali<br>• Kupoteza ardhi ya kilimo<br>• Upotevu wa malisho ya wanyama<br>• Kupoteza mazao na Kuanguka kwa miti | • Jamii<br>• misitu na miti ya asili | Maeneo ya pwani Mashariki na Magharibi na kwenye visiwa vidogo vidogo |

Wilaya ya Micheweni itaendelea kuathirika na majanga yaliyotajwa katika Jadweli Namba1 hadi Namba 3 pamoja na mengine yanayoweza kutokea siku zijazo. Utoaji wa tahadhari kwa umma pamoja na shughuli nyengine za kujiandaa zinaweza zikafanywa mapema kabla ya matukio mengi kutokea. Hata hivyo, baadhi ya majanga hutokea bila ya ishara yoyote au huwa ni ya muda mfupi. Kwa vile huchukua muda mrefu kupata msaada kutoka nje, ni muhimu kwa wilaya kujiandaa mapema ili kuweza kukabiliana na hali itakayojitokeza.

## 7 TARATIBU ZA OPERESHENI

Mpango huu umeelezea kazi mbalimbali zinazotakiwa kufanywa wakati wa hali ya dharura kwa taasisi mbalimbali za Serikali, zisizo za kiserikali na mashirika ya kujitolea katika ngazi ya wilaya ambazo zitafanywa sambamba na kazi zao za kawaida za kila siku kadri itakavyowezekana. Wafanyakazi na rasilimali hizo hizo zitatumika kwa kazi za kawaida na kazi za dharura. Kazi za kawaida za kila siku ambazo hazihusiani na masuala ya dharura zinaweza kusitishwa kwa muda wakati wa hali ya dharura.

Ikiwa hali ya dharura itakuwa iko juu ya uwezo wa wilaya wa kukabiliana nayo, na mpango wa Wilaya (MKKMWM) hautofanya kazi na hali ya dharura imetangazwa kuwa ni ya kitaifa, Mpango wa Taifa wa Kujiandaa Kukabiliana na Maafa utachukua nafasi. Mashirika na idara za Serikali zilizomo ndani ya wilaya zitahitajika kuchukua hatua haraka za kukabiliana na hali pamoja na timu za uokozi za taifa. Viongozi wa Serikali ya wilaya lazima wajue uwezekano wa kutokea hali ya dharura au maafa makubwa na lazima wajue majukumu yao katika utekelezaji wa mpango huu.

Ni wajibu wa Serikali ya wilaya kusimamia kikamilifu mpango ambao utakidhi mahitaji ya dharura kwa wale ambao ama wameathirika au wanaweza kuathirika kutokana na hali ya dharura au maafa makubwa. Inajulikana kwamba wilaya ina uwezo mdogo wa rasilimali katika kukabiliana na hali ya dharura. Hata hivyo, pamoja na wilaya kuwa na rasilimali kidogo, ikiwa zitatumika kwa umakini, zinaweza kupunguza upotevu

wa maisha na uharibifu wa mali wakati wa tukio la dharura au maafa makubwa. Hii ni pamoja na kushirikiana na sekta binafsi, taasisi zisizo za kiserikali, jumuiya ya kimataifa pamoja na mashirika ya kujitolea. Idara ya Kukabiliana na Maafa na Kamati ya kukabiliana na Maafa ya Wilaya zitakuwa na jukumu la kukusanya rasilimali kwa ajili ya shughuli za operesheni wakati wa dharura.

## SEHEMU YA PILI

## 8.0 MGAWANYIKO WA MAJUKUMU

### 8.1 UTANGULIZI

Sehemu hii inaainisha mgawanyiko wa majukumu kwa kila idara, mamlaka, taasisi binafsi, taasisi za kiraia na jumuiya za kujitolea zilizo katika Mpango wa Kujiandaa, Kukabiliana na Maafa wa wilaya ya Micheweni (MKKMWM).

### 8.2 MAJUKUMU

MKKMWM ni mpango unaotoa majukumu kwa taasisi, idara na mamlaka zote zilizo katika wilaya kutekeleza majukumu yao ya kila siku sambamba na miongozo ya shughuli zao. Shughuli hizi zitachangia katika harakati na operesheni za kujiandaa na kukabiliana na maafa katika wilaya.

Kamati ya maafa ya wilaya (KMW) inapoona kuwa maafa yaliyotokezea yamezidi uwezo walionao katika wilaya, watatoa taarifa hizo kwa Idara ya Kukabiliana na Maafa. Katika hatua hii taratibu na miongozo yote iliyomo katika Mpango wa Kitaifa wa Kujiandaa Kukabiliana na Maafa (MKKMZ) zitatumika mara baada ya kutangazwa kwa hali ya maafa kitaifa.

Taratibu na miongozo kwa mujibu wa majukumu ya taasisi yameelezwa katika kiambatanisho A Muhtasari wa shughuli hizo ni kama ufuatavyo:

1. Muongozo na udhibiti
2. Mawasiliano na tahadhari
3. Kuhamisha walioathirika kwenda katika eneo la usalama
4. Kuzima moto
5. Kusimamia haki na sheria
6. Huduma za afya na tiba
7. Utafutaji na Uokozi
8. Huduma za makaazi
9. Utoaji wa Taarifa za dharura kwa jamii
10. Ufanyaji wa tathmini ya uharibifu
11. Kazi za ufundi na uhandisi
12. Nishati na huduma nyenginezo
13. Udhibiti na usambazaji wa rasilimali
14. Usafirishaji

## 8.3 Mgawanyo wa majukumu kwa mujibu wa shughuli za taasisi

Mgawanyo wa majukumu kwa mujibu wa shughuli za taasisi utatekelezwa na taasisi husika kwa kutumia wafanyakazi na rasilimali walizonazo kwa shughuli za dharura katika wilaya. Taasisi hizo ni pamoja na:

i. Mashirika na Idara zilizoko wilayani
ii. Wadau wakuu na wahisani
iii. Taasisi zisizo za Serikali
iv. Kamati za maafa

**i. Mashirika na Idara zilizoko wilayani**

1. Mipango na takwimu
2. Afya
3. Kilimo
4. Mazingira
5. Elimu
6. Mifugo
7. Misitu
8. Uvuvi
9. Ustawi wa Jamii
10. Maendeleo ya wanawake na watoto
11. Vusajili wa vizazi na vifo
12. Usafirishaji
13. Ujenzi
14. Mratibu wa shughuli za Serikali
15. Afisa maafa wa Wilaya
16. Halmashauri ya wilaya

**ii. Wadau wakuu na wahisani**

1. Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar:
a. Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM)
b. Kikosi cha Zimamoto na Uokozi
c. Kikosi cha Mafunzo
d. Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU)
e. Kikosi cha Valantia
2. Jeshi la Polisi Tanzania
3. Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ)

4. Idara ya uhamiaji
5. Usalama wa Taifa
6. Wengineo

**iii. Taasisi zisizo za Serikali**

- Jumuiya za watu binafsi
- Jumuiya ya wafanyabiashara, wenye viwanda na wakulima
- Jumuiya ya wakulima wa karafuu Zanzibar
- Vyama vya ushirika
- Jumuiya ya Madereva Kaskazini Pemba (JMKP)

**Jumuiya zisizo za kiserikali**

- Muungano wa Jumuiya za kiraia Pemba
- Jumuiya ya kutoa misaada Pemba
- Jumuiya ya mayatima na kudhibiti Ukimwi ya wilaya
- Jumuiya ya kuhudumia jamii ya Micheweni
- Jumuiya ya kuhifadhi yam situ wa Ngezi
- Jumuiya ya Wanawake Kaskazini Pemba(JUWAKAP)
- Jumuiya ya Wazalishaji Mwani Pemba (JUWAMWAP)
- Mtandao wa Taasisi za Kiraia za Mkoa
- Jumuiya ya Maendeleo ya Konde
- Jumuiya ya Uhifadhi wa Misitu na Maliasili Micheweni (JUMMUMI)

**Taasisi za Kiraia za Kimataifa**

- Save the Children
- Millennium Village
- Action Aid
- Care International
- Community Forest

**Jumuiya za kidini**

- Istiqama
- Jumuiya ya maendeleo ya kiislamu ya kudhibiti mazingira na Ukimwi
- Jumuiya ya Maimamu Zanzibar (JUMAZA)
- Jumuiya ya Uamsho na Mihadhara ya Kiislamu (JUMIKI)
- Jumuiya ya kiislamu ya huduma za jamii

**Jumuiya za kijamii**

- Kamati za maendeleo za Shehia
- Vilabu vya michezo
- Jumuiya ya maendeleo ya Kiuyu Maziwang'ombe
- Jumuiya ya maendeleo ya Makangale

**v. Kamati za maafa**

Kamati ya Maafa ya Wilaya

Kamati ya Maafa ya Shehia

## 8.4 MGAWANYO WA MAJUKUMU

Katika mpango huu, mgawanyiko wa majukumu unategemea zaidi wajibu na majukumu ya taasisi za Serikali na mashirika yaliyoko wilayani. Kufanikiwa kwa operesheni za kukabiliana na maafa zinahitaji jitihada za pamoja kutoka kwa wadau wote. Ili kuimarisha jitihada za uratibu wa maafa mpango huu umeelezea majukumu hayo kwa kuzipa taasisi zote wajibu wa msingi na wajibu saidizi ili ziweze kutekeleza shughuli zao. Kijumla taasisi zilopewa majukumu ya msingi zitakuwa ni taasisi kiongozi na nyengine zitakuwa taasisi saidizi na taasisi hizo zitatekeleza wajibu wao kulingana na ujuzi na taaluma zao. Jadweli namba 4 linaonyesha majukumu ya taasisi, mashirika na jumuiya.

**Jadweli Namba 4: Shughuli za kujiandaa na kukabiliana na maafa**

| Kabla ya maafa | Wakati wa maafa | Baada ya maafa | Wahusika |
|---|---|---|---|
| **Ukame:**<br>• Kuanzisha vikundi vya wakulima.<br>• Utoaji wa taarifa za tahadhari.<br>• Kuvitambua vyanzo vya maji vya uhakika.<br>• Kuweka akiba ya chakula.<br>• Kuwaelimisha wakulima juu ya matumizi ya mbegu zinazostahamili ukame na za muda mfupi.<br>• Kutekeleza mkakati wa Serikali wa kilimo cha umwagiliaji maji.<br>• Uvunaji wa maji ya mvua kwa ajili ya umwagiliaji na mifugo. | • Kufanya tathmini ya haraka ya kujua mahitaji yaliopo kutokana na uharibifu uliotokea.<br>• Kutoa msaada wa huduma za chakula.<br>• Kutoa chakula cha dharura kwa watoto.<br>• Ugawaji wa mbegu zinazostahamili ukame | • Kufanya tathmini ya uharibifu uliotokezea.<br>• Kufanya utafiti juu ya mbegu zinazostahamili ukame.<br>• Kutoa huduma za ugavi.<br>• Kutoa msaada wa pembejeo za kilimo.<br>• Kusambaza mbegu za muda mfupi. | **Taasisi kiongozi:**<br>• Idara ya Kilimo<br>**Taasisi saidizi:**<br>• Idara ya Kukabiliana na Maafa<br>• Kamati za maafa za Wilaya na Shehia<br>• Mamlaka ya maji (ZAWA)<br>• Taasisi za kiraia na watu binafsi.<br>• Jumuiya za JUMMUMI, NGENARECO, ZACPO, Community Forest, |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Maradhi ya mripuko:**<br>• Kutoa elimu na kujenga uelewa kwa jamii.<br>• Kuandaa utaratibu wa ugavi na usafirishaji wa watu na vitu.<br>• Kuandaa taratibu za makaazi ya dharura.<br>• Upanuzi wa wodi katika hospitali za wilaya.<br>• Kuweka taratibu bora za kinga.<br>• Kuweka mfumo bora wa utoaji wa taarifa za tahadhari. | • Kufanya tathmini ya haraka ya kujua mahitaji yaliopo kutokana na uharibifu uliotokea.<br>• Utafutaji wa rasilimali (fedha, watu na vifaa)<br>• Kufukiza dawa maeneo yote yaliyoathirika.<br>• Kutoa uelewa kwa jamii juu ya athari za wadudu waharibifu.<br>• Kutoa elimu kwa jamii juu ya matumizi bora ya madawa ya kisasa na ya asili.<br>• Kuwafanyia uchunguzi wa kiafya walioathirika katika maeneo ya matukio.<br>• Kuhifadhi madawa na kuyasambaza kwa wahusika.<br>• Kuweka vituo vya kutoa na kupokea taarifa za walioathirika. | • Kufanya tathmini ya haraka ya tukio pamoja na walioathirika.<br>• Kuelimisha jamii<br>• Kutoa huduma za chanjo<br>• Kutoa taarifa | **Taasisi Kiongozi**<br>• Idara ya huduma za kinga na huduma za afya.<br>**Taasisi saidizi:**<br>• Idara ya Kukabiliana na Maafa<br>• Kamati za maafa za Wilaya na Shehia<br>• Kamati za afya za shehia<br>• Mamlaka ya Maji (ZAWA)<br>• Kuelimisha jamii, MISCO, DOACO, ISSO, MIDECAC, Chama cha Msalaba Mwekundu, Save the Children, UNICEF, vyombo vya habari. |
| | • Uhamishaji wa walioathirika kwenda katika maeneo salama.<br>• Uratibu wa shughuli za ugavi.<br>• Utambuzi wa waliofariki na kuandaa taratibu za mazishi. | | |
| **Wadudu waharibifu:**<br>• Kufanya maandalizi ya kikosi kazi cha wataalamu wa kilimo.<br>• Kuelimisha jamii na kutoa uelewa kwa jamii.<br>• Kuendelea kufanya utafiri juu ya wadudu waharibifu.<br>• Kudhibiti uingiaji wa mbegu ambazo hazijathibitishwa na mamlaka za kilimo.<br>• Kuzalisha mbegu za asili.<br>• Kuanzisha madarasa ya majaribio ya mbegu bora. | • Kufanya tathmini ya haraka ya kujua mahitaji yaliopo kutokana na uharibifu uliotokea.<br>• Utafutaji wa rasilimali (fedha, watu na vifaa)<br>• Kufukiza dawa maeneo yote yaliyoathirika.<br>• Kutoa uelewa kwa jamii juu ya athari za wadudu waharibifu.<br>• Kutoa elimu kwa jamii juu ya matumizi bora ya madawa ya kisasa na ya asili. | • Kufanya tathmini ya uharibifu uliotokezea.<br>• Kuangamiza na kuondoa mbegu zote zilizoathirika.<br>• Kutoa mbegu zinazostahamili ukame na za muda mfupi<br>• Kutoa huduma za ugavi na ushauri | **Taasisi Kiongozi:**<br>• Idara ya Kilimo<br>**Taasisi saidizi:**<br>• Idara ya Kukabiliana na Maafa<br>• Kamati za maafa za Wilaya na Shehia<br>• DFT, JUMMUMI, NGENARECO, MIDECAC, ZACPO, Community Forest |

| | | | |
|---|---|---|---|
| • Kuanzisha kituo cha uchunguzi wa mbegu, mbogamboga na matunda yanayotoka nje ya nchi.<br>• Kuandaa vifaa na madawa ya kutokomeza wadudu waharibifu. | | | |
| **Maradhi ya mifugo:**<br>• Kutoa elimu ya ufugaji kwa wafugaji.<br>• Ufanyaji wa mara kwa mara wa tafiti za magonjwa ya mifugo.<br>• Kufanya uchunguzi na kuthibitisha wanyama wanaotoka nje ya nchi na mazao yao.<br>• Kuanzisha vituo vya | • Kufanya tathmini ya haraka ya kujua mahitaji yaliopo kutokana na uharibifu uliotokea.<br>• Kuitisha kikosi kazi cha wataalamu kwa ajili ya kukabiliana.<br>• Utafutaji wa rasilimali (fedha, watu na vifaa) | • Kufanya tathmini ya uharibifu uliotokezea.<br>• Kutoa ushauri na huduma za ugani. | **Taasisi kiongozi:**<br>• Idara ya huduma na utibabu wa mifugo.<br><br>**Taasisi saidizi:**<br>• Idara ya kukabiliana na maafa.<br>• Kamati ya Maafa ya Wilaya<br>• Kamati za Maafa za Shehia |
| uchunguzi wa wanyama wanaotoka nje.<br>• Kuanzisha vituo vya chanjo katika Shehia.<br>• Kuweka tayari vifaa na madawa. | • Kutoa uelewa kwa jamii juu ya athari za magonjwa ya mifugo.<br>• Kuangamiza na kuondoa mifugo yote iliyoathirika na magonjwa hayo.<br>• Kuanzisha maeneo ya uchunguzi wa mifugo kwa muda. | | • |
| **Uchafuzi wa mazingira na kumong'onyoka kwa fukwe za bahari:**<br>• Kutoa elimu ya uhifadhi wa mazingira.<br>• Kufanya ukaguzi wa mara kwa mara katika maeneo hatarishi.<br>• Kusimamia kanuni na taratibu. | • Kufanya tathmini ya haraka ya kujua mahitaji yaliopo kutokana na uharibifu uliotokea.<br>• Kuitisha kikosi kazi cha wataalamu kwa ajili ya kukabiliana.<br><br>• Utafutaji wa rasilimali (fedha, watu na vifaa) | • Kufanya tathmini ya uharibifu uliotokezea.<br>• Kuanzisha mkakati wa kutoa muamko kwa jamii juu ya uhifadhi wa mazingira.<br>• Kufanya matengenezo na kuimarisha maeneo yaliyoathirika. | **Taasisi kiongozi:**<br>• Idara ya Mazingira<br><br>**Taasisi Saidizi:**<br>• Idara ya Kukabiliana na Maafa<br>• Kamati ya Maafa ya Wilaya<br>• Kamati za Maafa za Shehia<br>• Polisi Jamii<br>• Taasisi za kusimamia sheria<br>• Kamati za mazingira za Shehia<br>• Jumuiya mbalimbali kama vile; NGENARECO, JUMMUMI, KONDEO, JUMATU, KIMADO |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Upepo mkali:**<br>• Kutoa elimu juu ya athari za upepo mkali.<br>• Kuwatambua watu maarufu ambao wana taaluma ya kujua na kutabiri juu ya hali ya hewa kwa kutumia njia za jadi.<br>• Kuweka taarifa za hali ya hewa za asili na zile zinazotolewa na mamlaka ya Hali ya hewa.<br>• Kutoa taarifa za tahadhari kwa jamii.<br>• Kutoa elimu ya uokozi kwa jamii. | • Kufanya tathmini ya haraka ya kujua mahitaji yaliopo kutokana na uharibifu uliotokea.<br>• Kuandaa vikao vya kuratibu upatikanaji na utoaji wa rasilimali zinazohitajika.<br>• Kuendelea kutoa taarifa za tahadhari. | • Kufanya tathmini ya uharibifu uliotokezea.<br>• Kuandaa ripoti ya tukio na athari zilizotokea. | **Taasisi Kiongozi**:<br>• Idara ya Kukabiliana<br><br>**Taasisi Saidizi:**<br>• Mamlaka ya hali ya hewa.<br>• Mamlaka ya usafiri Baharini.<br>• Idara ya Uvuvi kamati ya Maafa ya Wilaya<br>• Kamati za Maafa za Shehia<br>• Kamati za uvuvi<br>• Jumuiya za ISSO, MISCO, NGENARECO |
| **Ajali za Baharini:**<br>• Kutoa elimu ya maafa kwa jamii.<br>• Kutoa taarifa za tahadhari kwa jamii.<br>• Kuweka taarifa za hali ya hewa za asili na zile zinazotolewa na mamlaka ya Hali ya hewa.<br>• Kutoa elimu ya uokozi kwa jamii.<br>• Frequent and spot inspections | • Kuitisha kikosi kazi cha wataalamu kwa ajili ya kukabiliana.<br>• Kuandaa vikao vya kuratibu upatikanaji na utoaji wa rasilimali.<br>• Kufanya operesheni ya kutafuta na kuokoa waathirika.<br>• Kutoa taarifa kwa jamii.<br>• Kuandaa huduma za utambuzi wa maiti na shughuli za mazishi. | • Kufanya tathmini ya uharibifu uliotokezea.<br>• Kusimamia haki na sheria | **Taasisi Kiongozi**:<br>• KMKM<br>• Mamlaka ya usafiri Baharini.<br><br>**Taasisi Saidizi:**<br>• Idara ya Kukabiliana na Maafa.<br>• Idara ya Uvuvi<br>• Kamati ya Maafa ya Wilaya<br>• Kamati za Maaafa za Shehia<br>• Jeshi la Polisi,<br>• Timu za afya za Wilaya Kamati za uvuvi za Wilaya<br>• Chama cha Msalaba Mwekundu.<br>• Shirika la Bima<br>• Jumuiya za ISSO, MISCO, |
| **Moto**<br>• Kutoa elimu juu ya athari na matumizi salama ya moto.<br>• Kuanzisha na kuimarisha vituo vya zima moto.<br>• Kuanzisha vituo vya maji kwa ajili ya kuzimia moto kila eneo.<br>• Kutoa elimu ya kuzima moto na uokozi.<br>• Kuanzisha huduma ya simu ya bure kwa masaa 24. | • Kuitisha kikosi kazi cha wataalamu kwa ajili ya kukabiliana.<br>• Kuhamisha walioathirika kwenda katika eneo salama | • Kufanya tathmini ya uharibifu uliotokezea.<br>• Kutoa huduma za misaada na Bima | **Taasisi Kiongozi:**<br>• Kikosi cha Zimamoto na Uokozi<br>**Taasisi Saidizi**:<br>• Jeshi la Polisi<br>• Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania<br>• Idara Maalum za Serikali (KMKM, JKU, Valantia, Mafunzo)<br>• Kamati ya Maafa ya Wilaya<br>• Kamati za maafa za Shehia<br>• Idara ya Mazingira<br>• Idara ya Misitu na Mali zisizorejesheka. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | • Shirika la Bima<br>• Shirika la Umeme<br>• Jumuiya za NGENARECO, Community Forest, ZACPO, |
| **Mvua kubwa na Mafuriko:**<br>• Kutoa elimu na uelewa juu ya athari za mvua kubwa na mafuriko na namna bora ya kujikinga.<br>• Utafutaji wa rasilimali na vifaa muhimu vya dharura.<br>• Kuandaa eneo la kuhifadhi watakaoathirika na mafuriko yatakapotokea.<br>• Kuimarisha miundombinu.<br>• Kuimarisha mfumo wa tahadhari za awali.<br>• Kutoa taarifa za tahadhari | • Kufanya shughuli za uokozi wa watu na mali zao.<br>• Utafutaji wa rasilimali (fedha, watu na vifaa)<br>• Kufanya tathmini ya haraka ya mahitaji. | • Kufanya tathmini ya uharibifu uliotokezea.<br>• Kutoa huduma za misaada na Bima | **Taasisi Kiongozi:**<br>• Kamati ya Maafa ya Wilaya<br><br>**Taasisi Saidizi:**<br>• Idara ya kukabiliana na Maafa<br>• Kamati za maafa za Shehia<br>• Idara ya Kilimo<br>• Idara ya Mazingira chama cha Msalaba Mwekundu<br>• Idara ya Ustawi wa jamii<br>• Timu ya afya ya Wilaya<br>• Shirika la Bima<br>• Shirika la Umeme<br>• Mamlaka ya maji<br>• Idara ya Mawasiliano na Miuondombinu |
| **Ajali za Barabarani:**<br>• Kutoa elimu na uelewa juu ya namna bora ya kutumia barabara na jinsi ya kujikinga na ajali.<br>• Kusimamia kanuni na taratibu za usalama barabarani.<br>• Kuweka alama za barabarani na hasa maeneo ya mkusanyiko.<br>• Kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa vyombo na miundombinu ya barabara. | • Kutoa huduma ya kwanza<br>• Kutoa huduma za matibabu kwa waliojeruhiwa.<br>• Kufanya tathmini ya haraka ya mahitaji.<br>• Kutoa taarifa kwa jamii | • Kufanya tathmini ya kina ya tukio.<br>• Kutoa huduma za Bima<br>• Kuweka kumbukumbu. | **Taasisi kiongozi**:<br>• Jeshi la Polisi<br>• Hospitali za Wilaya<br><br>**Taasisi Saidizi**:<br>• Idara ya Mawasiliano na Miundombinu<br>• Kamati ya Maafa ya Wilaya<br>• Kamati ya maafa za Maafa za Shehia<br>• Idara maalum za Serikali<br>• Halmashauri ya Wilaya<br>• Timu ya afya ya wilaya<br>• Jeshi la Polisi<br>• Wizara ya Elimu<br>• Shirika la Bima |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Kupanda kwa maji ya bahari katika maeneo ya juu.**<br>• Kutoa elimu ya mazingira<br>• Kusimamia matumizi salama ya fukwe na mikoko.<br>• Kusimamia kanuni na sheria. | • Kufanya tathmini ya haraka ya athari na mahitaji.<br>• Kuhamasisha upandaji wa miti ya mikoko | • Kusimamia utekelezaji wa mikakati ya uhifadhi wa fukwe. | **Taasisi Kiongozi:**<br>• Idara ya Mazingira<br><br>**Taasisi Saidizi:**<br>• Idara ya Misitu na mali zisizorejesheka.<br>• Kamati za mazingira za Shehia.<br>• Mradi wa SMOLE<br>• Jumuiya za NGENARECO, Community Forest, |

## 8.5 Uwezo wa wilaya juu ya Rasilimali za maafa

Uwezo wa Wilaya juu ya Rasilimali za maafa ni mdogo sana hususani rasilimali fedha, hii inatokana na ukweli kuwa asilimia kubwa ya mapato hukusanywa na Taasisi na Mashirika ya Serikali. Kwa upande wa vifaa na rasilimali nyengine Wilaya inazo baadhi ya rasilimali hizo ambazo zinaweza kusaidia wakati wa dharura na maafa. Rasilimali hizo ni pamoja na; vituo na huduma za afya, majengo ya skuli, vituo vya Polisi, usafiri na nyenginezo.

Jadweli lifuatalo linaonyesha muhtasari wa tathmini ya rasilimali za wilaya kulingana na aina ya majanga na maafa zitakazotumika kabla na wakati na baada ya maafa hayo.

**Jadweli namba 5: Tathmini ya rasilimali za wilaya**

| Aina ya rasilimali | Maelezo ya rasilimali hizo | Eneo zilipo | Mmiliki | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| Huduma za afya | • Vituo 13 vya afya.<br>• Hospitali ya Wilaya 1<br>• Wafanyakazi 122 wa kutoa huduma. | Micheweni | Serikali | Wakati wa maafa vituo hivyo na wafanyakazi hao hutumika kutoa huduma za matibabu. |
| Majengo ya skuli | Zipo jumla ya skuli 33 zenye vyumba vya kutosha | Micheweni | Serikali | Majengo ya skuli huweza kutumika kama makaazi ya muda wakati wa dharura na maafa. |
| Maghala ya kuhifadhia vifaa | Lipo ghala moja tu | Wete | Serikali | Inapotokea dharura ghala lililopo Wete ndilo ambalo linaweza kutumika kuhifadhia na kusambaza vifaa. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Vifaa na huduma za kuzimia moto | Hakuna kituo cha kuzimia moto ndani ya wilaya, hata hivyo, vipo vituo vitatu vya maji ambavyo magari ya kuzimia moto huweza kuchukua maji kwa ajili ya operesheni zao. | Chake Chake | Serikali | Maofisa wa zimamoto kutoka Chakechake ndio ambao huitwa kwa ajili ya kutoa huduma. |
| Vyanzo vya maji | Vipo vituo vitatu vya maji ambavyo magari ya kusambazia maji huweza kuchukua maji na kupeleka sehemu husika. | Micheweni | Serikali | Mamlaka ya maji husambaza maji katika maeneo yote ya makaazi wakati wa dharura. |
| Usafirishaji | Kuna jumla ya magari 98 ya kusafirishia abiria na mizigo. | Micheweni | Sekta Binafsi | Vyombo vya usafiri vya Serikali na binafsi hutoa huduma wakati wa dharura. |
| Vituo vya Polisi na Usalama | Kuna vituo viwili (2) vya Polisi na kambi mbili (2) za FFU, kambi moja (1) ya Jeshi (JWTZ) kambi moja (1) ya (JKU) na kambi moja (1) ya KMKM | Micheweni | Serikali | Vikosi hivi vya ulinzi na usalama husaidia sana kutoa huduma za uokozi wakati wa dharura. |
| Huduma za chakula na bidhaa nyengine | Kuna idadi ndogo ya wafanyabiashara za vyakula na bidhaa nyengine wa jumla, hata hivyo wafanyabiashara ya reja reja wapo wa kutosheleza | Micheweni na Wete | Sekta binafsi | Idara ya Usalama na Uhakika wa CHakula na Lishe watasaidia kutoa na kusambaza chakula wakati itakapohitajika. |
| Fedha | Serikali ya wilaya hukusanya kodi na mapato ndani ya wilaya. | Micheweni | Serikali | Fedha hizo husaidia wakati wa dharura ingawaje ni kwa kiasi kidogo |

## SEHEMU YA TATU

### 9.0 MKAKATI WA UTEKELEZAJI WA MPANGO

### 9.1 UTEKELEZAJI

Mpango wa Kujiandaa, Kukabiliana na Maafa wa Wilaya ya Micheweni (MKKMWM) utatekelezwa sambamba na Mipango ya Wilaya ya sekta zote na ni lazima ziingize masula ya maafa katika mipango yao wakati watakapofanya mapitio ya mipango hiyo. Taasisi na mashirika yote tatatekeleza shughuli zao za kawaida sambamba na shughuli zilizoainishwa katika mpango huu. Mpango huu utafanyiwa mapitio kila mwaka na wajumbe wote wa Kamati ya Maafa ya Wilaya watatakiwa kutoa michango yao. Hivi sasa Serikali inaifanyia marekebishoSera ya Serikali za Mitaa ambapo mambo mengi yanaweza kubadilika, mambo hayo ni pamoja na muundo, majukumu na shughuli za Serikali za mitaa. Kwa mnasaba huu mabadiliko hayo ni vyema yahusishwe katika mpango huu na yasiathiri utekelezaji wake.

### 9.2 MKAKATI MAALUM

Mkakati maalum uliokusudiwa katika kuandaa Mpango wa Kujiandaa Kukabiliana na Maafa ni kupunguza kwa kiasi kikubwa vifo na upotevu wa mali. Watendaji wa Kamati ya Maafa ya Wilaya, Sekta binafsi, Taasisi zisizo za Serikali na Jumuiya za kiraia na taasisi nyengine wanapaswa kushirikiana katika kutekeleza majukumu yao katika kujikinga na maafa. Majukumu ya kukabiliana na maafa yamegawika katika sehemu kuu tatu (3)

i. Kabla ya Maafa
ii. Wakati wa Maafa
iii. Baada ya Maafa.

**Kabla ya maafa (wakati wa kujiandaa – kabla ya maafa)**

Katika kipindi hiki mambo muhimu ya kuzingatia ni

- Kuimarisha Kamati ya Maafa ya Wilaya na zile za Shehia
- Kuhusisha mpango huu na mipango ya sekta.
- Kuandaa mipango ya utekelezaji wa shughuli za maafa
- Kufanya utafiti na uchambuzi wa majanga yanayoweza kutokea
- Kugawa majukumu kwa kila mmoja, kikundi , taasisi, jumuiya pamoja na taaasisi za kujitolea
- Kuweka utaratibu na program za kuelimisha jamii kwa kutumia njia mbalimbali

- Kutoa mafunzo ya kujenga uwezo
- Kuweka utaratibu mzuri wa masuala ya ugavi pamoja na kuainisha maeneo ya makaazi ya muda wakati wa maafa.
- Kuweka akiba ya vifaa na bidhaa muhimu kama vile Chakula, madawa, mavazi na mengineyo.
- Kuweka mtandao mzuri wa mawasiliano
- Kuweka orodha ya watendaji na wadau wote pamoja na uwezo na nyenzo walizonazo.

**Wakati wa Maafa**

- Utoaji wa taarifa za tahadhari
- Kufanya vikao vya uratibu na watendaji wa Idara
- Kuwapa taarifa watendaji wa sekta zote mara baada ya kutangazwa kwa maafa ili waweze kutoa huduma kwa haraka.
- Kutoa huduma za kibinaadamu kwa haraka.
- Kuhakikisha kuwa huduma zote muhimu zinawekwa katika maeneo ya kuokolea.
- Kusimamia vituo vya uokozi.
- Kusimamia na kuongoza shughuli zote za kukabiliana na maafa hayo.
- Kusimamia utoaji na uingiaji wa misaada.
- Kusimamia haki na Sheria
- Kuanda ripoti za tukio za kila siku.

**Baada ya Maafa**

- Kufanya tathmini ya hasara na athari zinazojitokeza
- Kusimamia na kusambaza misaada kwa walioathirika.
- Kuanzisha tena mifumo imara ya kijamii, kiuchumi
- Kuhakikisha kuwa usafiri wa uhakika unakuwepo kusafirishia bidhaa
- Kuhakikisha kuwa usalama wa walioathirika na mali zao unapatikana muda wote
- Kusimamia haki na sheria
- Kuhakikisha familia zilizopoteana zinakutanishwa na kurudi majumbani kwao.
- Kutoa huduma maalum kwa wazazi wanaonyonyesha, watoto na wazee
- Kukusanya na kuhifadhi taarifa za tukio.

Mkakati uliweka katika ngazi ya Wilaya ni lazima uoanishwe na mikakati iliopo katika ngazi ya Kitaifa kwa kufuata muundo uleule uliowekwa na serikali za mitaa wakati mchakato wa mabadiliko yanaendelea. Matukio ya maafa yanapozidi uwezo wa wilaya kukabiliana nao, hivyo Mpango wa Kukabiliana na Maafa wa Zanzibar utatumika.

## KIAMBATANISHO

**Kazi na Majukumu**

**I. Muongozo na Udhibiti**

Taasisi Kiongozi: jukumu la msingi la kusimamia shughuli hii litasimamiwa na Kamati ya Maafa ya Wilaya.

**Taasisi Kiongozi:** Kamati za Maafa za Shehia

**Shughuli za kutekeleza:**

i. Kuanzisha sera itakayoweka mikakati ya kusimamia program za maafa.
ii. Kusimamia shughuli zote za kukabiliana na maafa na kutoa miongozo pale inapohitajika.
iii. Kutoa taarifa kwa jamii juu ya maafa yaliyotokea kwa msaada wa Kitengo cha Habari na Elimu
iv. Kuelekeza utendaji wa Kituo cha Operesheni za dharura
v. Kuandaa mpango utakaoonyesha mahitaji ya watendaji, vifaa na mahitaji.
vi. Kupanga majukumu na kazi za Idara, mashirika na jumuiya za kujitolea.
vii. Kuratibu shughuli za kujiandaa na kuimarisha mpango huu.
viii. Kuandaa mafunzo kwa watendaji wa wilaya na taasisi nyengie za kukabiliana na maafa.

**II. Mawasiliano na tahadhari**

Taasisi Kiongozi: jukumu la msingi kwa shughuli hii litasimamiwa na Kamati ya Maafa ya Wilaya.
Taasisi Saidizi: Kamati za Maafa za Shehia, Mamalaka ya Hali ya Hewa, Idara ya Mawasiliano, Kamisheni ya Utalii, Jeshi la Polisi, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania,vyombo vya habari (Televisheni, redio na magaazeti) Radio za jamii, makampuni ya simu, Mamlaka ya Usafiri baharini, Taasisi ya Sayansi za Bahari na Chama cha Msalaba Mwekundu.

**Shughuli za kutekeleza:**

- Kupokea taarifa za hali ya dharura.
- Kuwatahadharisha watendaji juu ya tukio la dharura.
- Kutoa tahadhari na maelekezo kwa kutumia mfumo wa tahadhari uliopo.
- Kutoa tahadhari na maelekezo kwa skuli, vyuo vya mafunzo, vituo vya wazee na malezi ya watoto na hospitali.
- Kuainisha mifumo ya mawasiliano iliopo nchini katika ngazi zote ili kuhakikisha kuwa imeunganishwa na inafanya kazi.
- Kuandaa mipango na taratibu za mawasiliano ya mifumo mbalimbali ya mawasiliano wakati wa dharura.

**III. Kuhamisha walioathirika kwenda katika eneo la usalama**

Taasisi Kiongozi: Jukumu la msingi kwa shughuli hii litasimamiwa na Kamati ya Maafa ya Wilaya na Jeshi la Polisi.

Taasisi Saidizi: Kamati za Maafa za Shehia, Kamisheni ya Utalii, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, Idara maalum za Serikali (Zimamoto na Uokozi, JKU, KMKM, KVZ and Mafunzo), Mamlaka ya Usafiri baharini, idara ya usafiri na leseni Chama cha Msalaba Mwekundu na Mashirika ya Kimataifa.

**Shughuli za kutekeleza:**

- Kuainisha maeneo ambayo yameshawahi kutumika kama eneo la makaazi ya muda katika matukio yaliyopita, au linaloweza kutumika.
- Kuweka mpango wa kuhamisha walioathirika katika maeneo yote yaliyoainishwa ikiwa ni pamoja na njia na mahitaji mengine ili kupunguza msongamano wa watu.
- Kuandaa taratibu zitakazorahisisha zoezi la uhamishaji kwa haraka.
- Kuweka mahitaji yanayohitajika kutoa taarifa za dharura kwa jamii
- Kuweka mpango wa kuhamisha walioathirika kwa maeneo maalum kama vile skuli, nyumba za kulelea watoto na wazee, hospitali na maeneo mengine.
- Kuweka utaratibu wa kuwasaidia waathirika kupata usafiri wanapohitaji wakati wa kuhama.

## IV. Kuzima moto

Taasisi Kiongozi: Jukumu la msingi kwa shughuli hii litasimamiwa na Zimamoto na Uokozi.

Taasisi Saidizi: Kamati za Maafa za Shehia, Kamisheni ya Utalii, Jeshi la Polisi, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, Idara maalum za Serikali ( JKU, KMKM, KVZ and Mafunzo), Mamlaka ya Usafiri baharini, idara ya usafiri na leseni Chama cha Msalaba Mwekundu na Mashirika ya Kimataifa.

**Shughuli za kutekeleza:**

- Kujiandaa na shughuli za kinga ya moto
- Kudhibiti moto unapowaka
- Kukabiliana na matukio yanayosababishwa na bidhaa hatarishi na umwagikaji wa mafuta
- Kukabiliana na matukio ya ugaidi.
- Kusaidia katika shuhuli za kuhamisha walioathirika.
- Kufanya tathmini ya uharibifu uliotokezea baada ya maafa.
- Kufanya ukaguzi wa vifaa vya kuzimia moto katika makaazi ya muda.
- Kuweka rekodi ya vifaa vya kuzimia moto.

## V. Kusimamia haki na sheria

Taasisi Kiongozi: Jukumu la msingi kwa shughuli hii litasimamiwa na Jeshi la Polisi.
Taasisi Saidizi: Kamati ya Maafa ya Wilaya na Kamati za Maafa za Shehia, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, Idara maalum za Serikali (Zimamoto na Uokozi, JKU, KMKM, KVZ and Mafunzo)
Shughuli za kutekeleza:

- Kuzuwia na kudhibiti msongamano wa watu kwenye matukio.
- Kukabiliana na matukio ya kigaidi.
- Kuimarisha ulinzi na usalama katika maeneo yote.
- Kuingia na kuhudumia katika maeneo yaliyotokea maafa.
- Kusaidia katika shughuli za kutoa tahadhari kwa jamii.
- Kufanya tathmini ya uharibifu uliotokezea baada ya maafa.
- Kuandaa na kusimamia uwekaji wa kumbukumbu za kisheria.

## VI. Huduma za afya na tiba

Taasisi Kiongozi: Jukumu la msingi kwa shughuli hii litasimamiwa Idara ya Kinga na huduma za afya na hospitali za wilaya.

Taasisi Saidizi: Jeshi la Polisi, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, Idara maalum za Serikali (JKU, KMKM, KVZ and Mafunzo), idara ya Mazingira, Chama cha Msalaba Mwekundu, idara ya utibabu na huduma za mifugo, Mamlaka ya maji Zanzibar na Mashirika ya Kimataifa.

**Shughuli za kutekeleza:**

- Kutoa huduma za afya na matibabu wakati wa hali ya dharura.
- Kutoa elimu na taarifa za kiafya.
- Kuweka kanuni na taratibu za afya za dharura.
- Kuratibu shughuli za kutambua miili ya waliofariki na kusimamia mazishi.

## VII. Utafutaji na Uokozi

Taasisi Kiongozi: Jukumu la msingi kwa shughuli hii litasimamiwa Kikosi cha Zimamoto na uokozi na KMKM.

Taasisi Saidizi: Kamati za Maafa za Shehia, Jeshi la Polisi, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, Idara maalum za Serikali (JKU, KVZ and Mafunzo), Mamlaka ya Usafiri baharini, Mamlaka ya Viwanja vya ndege, idara ya usafiri na leseni, Chama cha Msalaba Mwekundu na Mashirika ya Kimataifa.

**Shughuli za kutekeleza:**

- Kuratibu shughuli za utafutaji wa waathirika na huduma za uokozi.
- Kuainisha mahitaji muhimu ya rasilimali kwa ajili ya shughuli za uokozi.
- Kuratibu na kutafuta msaada wa kiufundi na vifaa kutoka nje ya nchi.

## VIII. Makaazi na Huduma kwa walioathirika

Taasisi Kiongozi: Jukumu la msingi kwa shughuli hii litasimamiwa Kamati ya Maafa ya Wilaya.

Taasisi Saidizi: Kamati za Maafa za Shehia, Jeshi la Polisi, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, Idara Maalum za Serikali (JKU, KVZ and Mafunzo), Idara ya mipango miji na vijiji, Idara ya Upimaji na Ramani, Idara ya Ustawi wa Jamii, Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto, Idara ya Kilimo, Idara ya Kinga na huduma za afya, Chama cha Msalaba Mwekundu na Mashirika ya Kimataifa.

**Shughuli za kutekeleza:**

- Kuandaa mpango wa dharura wa makaazi na huduma za jamii
- Kuratibu shughuli za makaazi na huduma za jamii kwa kushirikiana na taasisi nyengine za misaada na vikundi vya kujitolea.
- Kuainisha vituo vya kutoa huduma za chakula.
- Kuainisha maeneo ya upatikanaji wa mavazi ya walioathirika.
- Kutafuta chakula na maji
- Kuratibu upatikanaji wa huduma muhimu kwa makundi maalum (watoto, wazee watu wenye ulemavu)
- Kutoa huduma za kisaikologia na ushauri nasaha kwa waliokumbwa na maafa.

## IX. Utoaji wa Taarifa za dharura kwa jamii

Taasisi Kiongozi: Jukumu la msingi kwa shughuli hii litasimamiwa Kamati ya Maafa ya Wilaya.

Taasisi Saidizi: Kamati za Maafa za Shehia, Jeshi la Polisi, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, Idara maalum za Serikali (JKU, KVZ and Mafunzo), Idara ya Mawasiliano, Idara ya Habari Maelezo, kampuni za simu (ZANTEL, Airtel, VODACOM, TIGO), vyombo vya habaro (Televisheni, Redio na Magaazeti) na Radio Jamii.

**Shughuli za kutekeleza:**

- Kuanzisha kituo cha habari cha pamoja.
- Kuandaa vipindi vya kuelimisha jamii
- Kuandaa taarifa na kuzitoa kwa jamii pamoja na maelekezo muhimu zinazohusiana na maafa.
- Kuandaa mikutano na vyombo vya habari.
- Kufuatilia na kusimamia vyombo vya habari ili kuhakikisha kuwa taarifa zinazotolewa ni sahihi.
- Kuandaa na kutoa taarifa za matukio ya maafa ikiwa ni pamoja na kuweka kumbukumbu za picha.

**X. Ufanyaji wa tathmini ya uharibifu**

Taasisi kiongozi: Idara ya Kukabiliana na Maafa na Kitengo cha mipango na utafiti ndio zenye jukumu la msingi kwa kazi hii.

Taasisi saidizi: Kamati za kukabiliana na maafa za shehia, Idara ya Ardhi na Usajili, Idara ya Mipango miji, Halmashauri ya wilaya, Idara ya ujenzi, Idara ya Mazingira na Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ).

**Shughuli za kutekeleza:**

- Kuanzisha na kukipatia mafunzo kikosi cha kufanya tathmini kilichoundwa na watu kutoka katika wilaya
- Kuratibu mipango ya kikosi cha kufanya tathmini kikiwa na wafanyakazi kutoka Idara ya Kukabiliana na Maafa
- Kutathmini na kukusanya taarifa juu ya hasara kwa mali za Serikali na za watu binafsi pamoja na mahitaji ya walioathiriwa, kutayarisha na kutekeleza mipango kukidhi mahitaji hayo.
- Ikiwa hasara iliyopatikana ni kubwa kuliko uwezo wa Serikali, taasisi husika zinatakiwa kukusanya taarifa zitakazotumika kuomba msaada katika Mashirika ya Kimataifa

## XI. Kazi za ufundi na uhandisi

Taasisi Kiongozi: Idara ya ujenzi ndio taasisi yenye jukumu la msingi kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hii

Taasisi saidizi: Idara ya usafiri na leseni, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Idara maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar

**Shughuli za kutekeleza:**

- Kuhifadhi vifaa na huduma muhimu za Serikali pale inapotakiwa kufanya hivyo
- Kufanya tathmini ya uharibifu katika maeneo ya makaazi, madaraja, vifaa vya usalama barabarani, pamoja na miundimbinu mingine ya umma
- Kusimamia matengenezo ya dharura ya vifaa na huduma muhimu kama vile umeme, maji, mawasiliano, miundombinu ya maji taka na usafirishaji. Huduma nyingine muhimu ikiwa ni pamoja na afya, polisi na huduma za zima moto na skuli.
- Kutengeneza barabara na madaraja yaliyoharibiwa
- Kutengeneza mifumo ya maji machafu
- Kupanga mipango ya uondoshaji wa kifusi
- Kutoa msaada wa jumla katika kufanya tathmini ya uharibifu
- Kusaidia shughuli za ukaguzi wa majengo
- Kutoa vifaa maalum kusaidia katika kazi za dharura
- Kusaidia kudhibiti msongamano wa watu pamoja na kazi za utafutaji na uokozi

## XII. Nishati na huduma nyinginezo

Taasisi kiongozi: Shirika la umeme Zanzibar (ZECO) ndilo lenye wajibu wa msingi kwa kazi hii

Taasisi saidizi: Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA), taasisi binafsi zinazojishighulisha na mambo ya nishati, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Idara maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar

**Shughuli za kutekeleza:**

- Kuweka kipaumbele katika kurudisha huduma ya nishati kwa maeneo yenye huduma muhimu
- Kutayarisha mipango ya kuweka vyanzo vya dharura vya nishati pale inapohitajika
- Kufanya tathmini ya uharibifu, matengenezo na kurudisha huduma muhimu kwa jamii
- Kusimamia kazi za kurudisha hali (baada ya dharura) kwa vifaa na huduma zinazomilikiwa na watu binafsi

## XIII. Udhibiti na Usambazaji wa Rasilimali

Taasisi kiongozi: Jukumu la msingi kwa kazi hii lipo kwa Idara ya Kukabiliana na Maafa na kitengo cha fedha na utawala katika Wizara ya Fedha.

Taasisi saidizi: Kamati za Kukabiliana na maafa za Shehia, Idara ya Kilimo, Halmashauri ya Wilaya, Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Shirika la Msalaba Mwekundu Zanzibar, Mashirika ya kikanda na ya kimataifa, Idara maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

**Shughuli za kutekeleza:**

- Kuendeleza ghala la vifaa vya dharura
- Wakati wa kazi za dharura kupeleka mahitaji, vifaa na nguvukazi kwa ajili ya kukidhi mahitaji
- Kuwa na orodha ya wasambazaji wa vifaa vinavyohitajika haraka wakati wa dharura
- Kutayarisha taratibu za dharura za manunuzi na kuratibu manunuzi kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya dharura
- Kuanzisha na kuweka nguvukazi ya ziada na kuratibu nguvukazi hizo kwa Idara na mashirika yanayozihitaji
- Kuratibu usafiri, upangaji, hifadhi ya dharura na usambazaji wa rasilimali wakati wa hali ya dharura.
- Wakati wa shughuli za dharura, ni muhimu kuainisha bidhaa na huduma pamoja na nguvukazi kwa mratibu aneyeshughulikia mambo ya misaada.
- Kuweka kumbukumbu za matumizi ya dharura kwa manunuzi na nguvukazi.

## XIV. Usafirishaji

Taasisi Kiongozi: Jukumu hili la msingi lipo katika Idara ya Usafirishaji na Leseni
Taasisi Saidizi: Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (ZAA), Mamlaka ya Usafiri wa Baharini (ZMA), Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Shirika la Msalaba Mwekundu Zanzibar na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar
Shughuli za kutekeleza:

- Kuainisha vyombo vya usafiri vya umma na vya watu binafsi na kuratibu matumizi yake katika shughuli za dharura, hasa katika kuhamisha walioathiriwa kutoka eneo la tukio kwenda maeneo ya usalama.
- Kuratibu shughuli za usambazaji wa vifaa kwa ajili ya kusaidia shughuli za dharura
- Kuanzisha na kuendeleza vikundi vya madereva wa akiba, mafundi, vipuri na vifaa
- Kuweka kumbukumbu za matumizi ya vyombo vya usafiri na nguvukazi.